

# TANGAZO LA AJIRA YA MUDA

Mkurugezi wa JIJI Dar es Salaam anawatangazia Watanzania wote wenye sifa nafasi ya kazi ya kukusanya ushuru wa vyoo

## I. WAKUSANYA USHURU WA VYOO VYA UMMA (NAFASI 42)

### SIFA ZINAZOHITAJIKA

- i. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne
- ii. Awe na elimu ya Cheti/ Stashahada ya Uhasibu au Uongozi wa Biashara kutoka Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

### KAZI/MAJUKUMU

- i. Kukusanya ushuru wa vyoo
- ii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake.

## 2. AFISA TEHAMA NAFASI (1) - (DDC)

### SIFA ZINAZOHITAJIKA

- i. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne
- ii. Awe na elimu ya Cheti/ Stashahada ya Tehama kutoka Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

## 3. DEREVA NAFASI (1) - (DDC)

- i. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne
- ii. Awe na cheti cha Udereva kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

### **3. WALINZI NAFASI (10) - (DDC)**

- i. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne
- ii. Awe amepata mafunzo ya Mgambo/JKT
- iii. Awe na sare za Mgambo

### **4. WAFANYA USAFI NAFASI 4. - (DDC)**

- i. Awe na uzoefu wa kufanya usafi
- ii. Awè na barua ya udhamini kutoka kwa mitumishi wa Serikali

#### **MASHARTI KWA UJUMLA:**

1. Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania.
2. Awe amehitimu na kupata cheti cha kidato cha Nne  
NB: "Results Slip" hazitakubadilika.
3. Awè na cheti cha kuzaliwa.
4. Awe na umri kati ya miaka 18-45.
5. Ajira ni ya mkataba wa miezi sita [6].
6. Mwajiri atalipa mshahara wa Tsh.10,000 kwa siku yenye kuleta jumla ya 300,000/= hadi 310,000/= kwa mwezi kwa Wakusanya Ushuru, Tehama, Dereva na Walinzi. Wafanya usafi watalipwa Sh.5,000/= kwa siku yenye kuleta jumla ya Sh.150,000/= kwa mwèzi.

#### **Barua zote ziambatane na nyaraka zifuatazo:**

- (i) Nakala za vyeti vya mwombaji vilivyothibitishwa ambayo ni:
  - Cheti cha kidato cha nne
  - Cheti cha Taaluma
  - Cheti cha Kuzaliwa.
  - Kitambulisho cha Taifa
- (ii) Picha ndogo ya rangi (colored Passport size moja ya hivi karibu ni).

(iii) Waombaji wenyе sifa pungufu au zaidi na zilizotajwa hapo juu hawaruhusiwi kuomba kwani maombi yao hayatafanyiwa kazi. Barua ambazo hazikuambatanishwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu hazitashughulikiwa.


#### **JINSI YA KUTUMA MAOMBI:**

Barua zote za maombi ziandikwé kwa mikonono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji pamoja na namba ya simu zitumwe kwa anuanini ifuatayo hapa chini;

**MKURUGENZI WA JIJI  
HALMASHAURI YA JIJI  
S.L.P. 20950  
DAR ES SALAAM.**

Mwisho kupokea maombi ni tarehe 27/03/2024 saa 9.30  
Mchana

Imetolewa na:

  
Mercedes Rusasa (Wakili)

KAIMU MKURUGENZI WA JIJI